
sababu wanapata kipato na wanaendesha maisha yao wengine wamenunua boda-boda," alisema.

HABARI LEO UK 18 June 17 2023



# Wakala yatakiwa kuongeza wigo elimu ya uvuvi

**Na Lucy Ngowi**

WAKALA ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imetakiwa kuongeza wigo wa ushirikiano katika kutoe elimu ya uvuvi.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Mohamed Shekh wakati akifunga mafunzo ya siku 30 ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa mazao ya samaki juu ya usalama, ubora na taratibu za ukaguzi kutoka nchini Somalia.

Profesa Shekh alisema kuwa Feta inatakiwa kuongeza wigo wa ushirikiano na nchi mbalimbali kwani zipo rasilimali nyingi na wataalamu wapo wa kutosha hivyo haitakiwi wataalamu kujifungia bali wajitokeze.

Alisema wataalamu wa uvuvi kutoka Somalia wamekuwa wakishiriki mafunzo hayo nchini kwa lengo la kuongeza uwezo katika kusimamia rasilimali za uvuvi na kuhakikisha kunakuwapo uvuvi endelevu nchini kwao.

Profesa Shekh alisema upo umuhimu mkubwa katika kuhakikisha mazao ya bahari yanakuwa na ubora unaotakiwa, hivyo aliitaka Feta kuhakikisha inaendelea kuhamasisha na kutoa mafunzo hayo kwa washiriki kutoka nchi mbalimbali.

Mtendaji Mkuu wa Feta, Dk Semvua Mzighani alisema lengo la mafunzo yanayotolewa chuoni hapo ni kufanya shughuli hizo kwa vitendo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wengine Rais wa wanafunzi hao kutoka Chuo cha Uvuvi Somalia, Elm Mohamed alisema kuwa ni vyema nchi zikashirikiana katika rasilimali kwani zinafanana.